JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU

# SERA BUNGE NA URATIBU

JARIDA LA MTANDAONI TOLEO LA NNE

APRILI 2023



## Waziri Mkuu: Tanzania kinara masuala ya Maafa

KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
2 BARABARA YA POSTA 40412 DODOMA TANZANIA



WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa amesema Tanzania imekuwa nchi ya kwanza kusaini mkataba wa kuanzisha Kituo cha Huduma za Binadamu na Operesheni za Dharura cha Kanda ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

"Lengo la kuanzisha kituo hicho ni kusimamia utoaji wa huduma na misaada ya kibinadamu kwa nchi wanachama. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, masuala ya majanga hayana mipaka na hayana muda na yanahitaji jitihada za pamoja katika kuyashughulikia," amesema.

Waziri Mkuu ametoa kauli hiyo wakati akiwasilisha hotuba kuhusu Mapitio na Mwelekeo wa Kazi za Serikali na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2023/2024.

"Kama mtakumbuka, katika kuendeleza uhusiano na nchi nyingine, hivi karibuni nchi yetu imeungana na mataifa mengine duniani kutoa misaada ya kibinadamu kwa nchi zilizopatwa na maafa makubwa yaliyosababisha vifo na majeruhi, uharibifu wa mali na mazingira. Nchi hizo ni Malawi iliyokumbwa na mafuriko yaliyosababishwa na kimbunga Freddy kilichotokea tarehe 13 Machi, 2023 na Uturuki iliyokumbwa na tetemeko la ardhi Februari, mwaka huu," amesema.

Ameitaja misaada iliyotolewa Malawi kuwa ni tani 1,000 za mahindi, mablanketi 6,000, mahema 50, fedha taslimu sh. milioni 705, dawa za binadamu na helikopta mbili kwa ajili ya kusaidia uokoaji. Vilevile, Uturuki ilipewa dola za Marekani milioni moja.

Akielezea utekelezaji wa shughuli za maafa kwa mwaka 2022/2023, Waziri Mkuu Majaliwa amesema wajumbe 555 wa Kamati za Usimamizi wa Maafa na Waratibu wa Maafa walipatiwa mafunzo ya kuimarisha uwezo wa utendaji kazi katika mikoa ya Arusha, Morogoro, Kilimanjaro, Lindi, Mtwara na Singida.

"Pia wavuvi 344 katika mwambao wa Ziwa Victoria na vijana 40 wa kujitolea katika mikoa ya Dodoma, Iringa, Songwe na Tabora walipata mafunzo ya uokoaji, yaliyowaongezea uwezo wa kukabiliana na maafa kwa wakati," amesema.

Amesema katika mwaka ujao wa fedha, Serikali itaendelea na ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Usimamizi wa Maafa jijini Dodoma na kuimarisha maghala ya vifaa vya misaada ya kibinadamu kwa kuongeza vifaa na kuendelea kutoa misaada kwa waathirika wa maafa.

Hata hivyo, Waziri Mkuu ameitaka kila wizara na taasisi wajiandae kwa vifaa vya kukabiliana na maafa kulingana na mahitaji ya wizara au taasisi husika.




# Matokeo ya Sensa yameonesha Tanzania imepiga hatua kimaendeleo-Majaliwa

WAZIRI MKUU, Kassim Majaliwa amesema kuwa matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 imeonesha Tanzania imepiga hatua katika kuwaletea maendeleo wananchi kwenye sekta mbalimbali ikiwemo Maji, Elimu, Afya, na Mawasiliano.

Amesema hayo wakati alipozindua Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, katika ukumbi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA)-Tunguu.

Hafla hiyo pia imehudhuriwa na Naye Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Seleman Abdulah.

Amesema kuwa katika Sekta ya Elimu, takwimu za Sensa zinaonesha kuwa kiwango cha jumla cha uandikishaji kwa wanafunzi ngazi ya shule za msingi kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kimefikia asilimia 95.9 Mwaka 2022 kutoka asilimia 94.6 ilivyokuwa Mwaka 2012.

“Kiwango cha kujua kusoma na kuandika kwa watu wenye umri wa miaka 5 na kuendelea kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kimeongezeka hadi asilimia 79.1 mwaka 2022 kutoka asilimia 72.0 ilivyokuwa mwaka 2012”.

Kadhalika, Waziri Mkuu amesema kuwa sekta ya maji matokeo ya Sensa yanaonesha kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea kufanya vizuri kwa kuwa asilimia 99.5 ya kaya zote zina vyanzo vya maji ambapo kati ya vyanzo hivyo asilimia 67.8 ni vyanzo vilivyoboreshwa na asilimia 32.2 ni vyanzo ambavyo havijaboreshwa.

Kwa upande wa mawasiliano, Mheshimiwa Majaliwa amesema kuwa takwimu zinaonesha kuwa asilimia 97.5 ya Vitongoji/Mitaa/Shehia vimefikiwa na mitandao ya simu. “Kiwango hiki kinafanana na hali ilivyo kwa Tanzania Bara. Wakati huohuo Tanzania Zanzibar imefanya vizuri zaidi kwa kufikia asilimia 99.0 ya shehia ambazo zimefikiwa na mitandao ya simu”.

Aidha, Waziri Mkuu amesema kuwa takwimu zinaonesha zaidi ya asilimia 50 ya Watanzania wote wapo kwenye umri wa miaka 15 hadi 64.

“Hii ni ishara nzuri katika maendeleo ya nchi, kidemographia umri huu unajulikana kama umri wa kufanya kazi Kwa maneno mengine, nchi yetu ina hazina kubwa ya nguvu kazi ambayo ni moja ya kichocheo katika kujenga uchumi imara”

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu ametoa rai kwa wananchi kufuatilia kwa karibu taarifa za usambazaji wa matokeo haya na kuyatumia katika kufanya maamuzi mbalimbali ya maendeleo ikiwa ni pamoja na kubaini maeneo ya uwekezaji, upatikanaji wa huduma za kijamii na maeneo ya masoko kulingana na mtawanyiko wa idadi ya watu nchini.



# Serikali yadhamiria Kuendelea Kuzingatia Masuala ya Utawala Bora

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulika na Sera Bunge na Uratibu Mhe. Jenista Mhagama amesema serikali imeridhia kuwa kifungu maalumu cha bajeti kwa ajili ya kuendesha baraza la Vyama Vya Siasa ili kuweza kufanya shughuli zake kwa ufanisi.

Kauli hiyo imetoloewa wakati wa Ufunguzi wa Kikao cha Baraza la Vyama Vya Siasa kilichofanyika Mjini Dar es salaam.

Amesema serikali Imepitisha Bajeti ya shilingi Billioni Shilingi 1,586,662,000.00 kwa ajili ya kuendesha baraza la Vyama Vya Siasa kwa Mwaka wa fedha 2023/24.

"Kwa kuwa sasa Mhe. Rais Dkt. Samia Sulluhu Hassan ameamua kutenga fedha ya kuendesha baraza, naomba vikao vyote vya kikatiba vya baraza la vyama vya siasa vikae kwa kwa mujibu wa ratiba ikiwa ni pamoja na vikao vya kamati kwa kufuata kanuni na sheria."

Ameongeza kusema baraza la vyama vya siasa lipewe nafasi ya kukutana serikali ili kujadiliana kuhusu mambo mabalimbali yanayohusu ustawi wa Demokrasia Nchini.

Iko miradi ya kimkakati hapa nchini, kuna kila sababu viongozi wa vyama vya siasa na baraza la vyama vya siasa wapate nafasi ya kuangalia miradihiyo , kwa sababu tunapofika kwenye masuala ya maendeleo ya nchi na ustawi nchi hakuna chama.

"kuna nafasi ya viongozi wa vyama vya siasa kutushauri vizuri zaidi kwa ustawi wa wananchi, "alisema Waziri Mhagama.

Aidha tunahitaji kutengeneza programu maalumu ya mafunzo kwa ajili ya viongozi wetu wa vyama vya siasa, ili tuendele kuimarisha Demokrasia ya vyama vingi chini, hatuwezi kufanikiwa kama viongozi wetu hawataendana na mabadiliko yanayoyendelea kwenye ulimwengu wa sasa.

Katika hatua nyingine Waziri Mhagama ameomba migogoro ya vyama imalizwe ndani ya vyama, tunauwezo wa kuimaliza sisi wenyewe, tujenge uwezo wa kutizama matatizo yetu ndani ya chama na kuyamaliza ndani ya vyama vyetu.

Waziri amehimiza viongozi wa vyama vya siasa, kuzingatia sheria za matumizi na mapato ya fedha.

Waziri Mhagama ametumia fursa hiyo kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kuboresha mfumo wa vyama vingi nchini Tanzania.

"Mhe. Rais alipoingia madarakani aliasisi " 4r" ambazo ni (reconcilian, resiliance, reform and rebuilding) kwa kiswahili ni maridhiano, ustamilivu, mageuzi na mabadiliko hii ikiwa ni kwa lengo la kutoa mwongozo wa jinsi ambavyo siasa za nchi yetu zinapaswa kuwa."

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Baraza la Vyama Siasa Juma Ally Khatibu, ameomba mfaunzo ya siku tatu mara tu baada ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ili kuwa na uelewa mkubwa kuhusu " 4r"



# WAZIRI MHAGAMA Ahimiza ubora ujenzi mnara wa mashujaa.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu Mhe. Jenista Mhagama amewataka wataalam kushirikiana na wakandarasi ili kuhakikisha ujenzi wa Mnara wa Mashujaa unakamilika katika viwango vyenye ubora.

Mhe. Mhagama ameyasema hayo wakati wa kikao chake na Wataalam, Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo Mbalimbali katika Ofisi hiyo waliokutana kwa lengo la kumpitisha katika ramani ya ujenzi wa Mnara huo katika kikao kilichofanyika Ukumbi wa Ofisi hiyo Jijini Dodoma.

Mhe. Mhagama amesema ujenzi wa Mnara huo kwa Awamu ya Kwanza unatarajiwa kugharimu shilingi Bilioni Moja ukitarajiwa kukamilika mapema kabla ya maadhimisho ya Mashujaa mwaka 2023.

"Kukamilika kwa Mnara huu itakuwa ni hatua kubwa sana kwa Serikali kama sehemu ya kuwakumbuka mashujaa wetu jinsi walivyoipigania Nchi yetu na utakuwa wa kipekee sana na nembo kubwa kwa Makao Makuu ya Nchi yetu Dodoma. Watanzania watapata fursa ya kutembelea hapo na kujifunza yaliyofanywa na Mashujaa wetu,"Amesema Mhe. Mhagama.

Vilevile Mhe. Mhagama amesisitiza matumizi sahihi ya fedha zilizotolewa na Serikali kukamilisha ujenzi huo kuhakikisha zinatumika kama ilivyopangwa ambapo kukamilika kwake kutafungua fursa nyingi za kiuchumi kutokana na miundo mbinu rafiki na huduma muhimu zitakazowekwa katika mnara huo.

Aidha amebainisha kwamba ujenzi wa Mnara huo ni sehemu ya utekelezaji wa maagizo ya Rais wa Jmahuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan aliyoyatoa wakati wa maadhimisho ya siku ya Mashujaa yaliyofanyika mwezi Julai mwaka 2022 ambapo aliagiza kujengwa kwa Mnara wenye ubora na hadhi ya makao makuu ya Nchi Dodoma.

.



# Sherehe za Maadhimisho ya Miaka 59 ya Muungano mwaka huu yafanyika kila mkoa

Kilele cha sherehe za Maadhisho ya miaka 59 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar Mwaka huu yamefanyika kiaina yake, ambapo kila mkoa unaadhimisha kwa kutelekeza maelekezo mahsusi ya Serikali.

Mkurugenzi wa Kitengo ya Maadhimisho na Sherehe za Kitaifa kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu Bw. Batholomeo Jungu ameyamesema hayo jana wakati ziara maalum ya Kamati ya Kitaifa ya maadhimisho hayo mwaka mwaka huu ilipotembelea na kukagua utekelezaji wa maelekezo mahsusi kwa Ofisi za Serikali Jijini Dodoma.

Bw. Jungu alisema kuwa kwenye mikoa ndipo kwenye wananchi hivyo shughuli hizi kufanyika katika mikoa zinaleta chachu ya uzalendo kwa wananchi sababu kila mtu anapata nafasi ya kushiriki kuanzia kwenye uzinduzi wa miradi, mashindano ya insha kwa wanafunzi, michezo mbalimbali, usafi wa mazingira na maswala mengine muhimu.

"Watu wapo katika kila mkoa, hivyo tukio hili la kushirikisha wananchi linaleta tija kwa jamii kwa kuona ni sehemu ya maadhimisho haya kwa vitendo,"alisisitiza Jungu.

Kwa Upande wake Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Bi. Mary Maganga aliseme

Kila mwaka tarehe 26 mwezi Aprili hututumika kama kumbukumbu ya sherehe za Muungano wa Iliyokuwa Tanganyika na Zanzibar, uliyofanya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, ambapo kaulimbiu ya Mwaka huu inasema " Umoja wetu na Mshikamano ndiyo nguzo ya kukuza uchumi wetu."

Katibu Mkuu Masanja alitumia fursa hiyo kueleza namna ofisi yake ilivyotekeleza maelekezo mahsusi ikiwemo kulipamba jengo la ofisi hiyo na kuweka picha za viongozi wakuu wa nchi pamoja na waasisi wa taifa leo

.

Jarida la Mtandao limeandaliwa na kutolewa na kitengo cha Mawasiliano Serikalini Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge na Uratibu.




KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
2 MTAA WA RELINI , S.L.P 980
40480 DODOMA
Baruapepe, ps@pmo.go.tz, simu, +255262322480
Fax;255262324534, Tovouti;www.pmo.go.tz